OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

12/04/2025 ► 18/04/2025

OAG

# Biteko aagiza mawakili watende haki

a Lidya Inda

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko ame-ataka mawakili wa serikali tenda haki wanapotekeleza ajukumu yao.

Aliyasema hayo jana odoma alipokuwa akifun-a Mkutano wa mwaka Chama cha Mawakili wa rikali na kuwataka kuifanya ki kuwa rafiki yao na si wa rafiki wa mtu.

"Mkatende haki ionekane ki inatendekea mikononi wenu, kila anayetoka mbele yenu atoke na tabasamu kuwa haki imetendeka ila atakayekosa haki atoke akiwa ameridhika kuwa kweli hakustahili kushinda," alisema Dk Biteko.

"Mtakapokuwa kwenye majukumu yenu, fanyeni kazi ya kuitetea serikali yenu maana ninyi ndio waanzishi wa mambo yote hata kama sheria zinatungwa zile zinazoanzia serikalini, anayetengeneza mchoro wa sheria ni timu hii," aliongeza.

Vilevile, aliwasisitiza wafanye kazi yao kwa kuzingatia maadili ya taaluma hiyo na wanapofanya kazi ya ushauri.

"Mshauri kwa haki bila kuogopa mtu katika kushauri kwenu ikiwa linamkwaza yule anayeshauriwa, fanya kazi yako ya kushauri halafu mwachie yeye aamue," alisema.

Alisema: "Katika masuala ya sheria, linaweza kutokea jambo unajua kabisa jibu ni hili lakini kwa sababu ya jukumu la pamoja unalirudisha kwa wenzako ili muamue kwa pamoja".

Dk Biteko aliwapongeza mawakili hao kwa utayari wao na kujitolea utaalamu kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki.

"Serikali inatambua jitihada mbalimbali za wizara na taasisi zake katika kutoa huduma kwa jamii, huduma ya sheria inayoendelea kutolewa kupitia Kampeni ya Msaada wa Sheria ya Mama Samia, kamati za ushauri wa sheria za mikoa na wilaya, kliniki za ushauri wa sheria ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufahamu kwa wananchi kuhusu utatuzi wa kisheria na utatuzi wa migogoro ya kisheria na hatimaye kuchangia ustawi wa jamii na kuimarisha amani nchini na kukuza uchumi," alifafanua.

Alisema katika kliniki zilizofanyika kwenye mikoa mbalimbali, malalamiko 398 yalisikilizwa na kati ya hayo, 167 yalikuwa ya ardhi.

Akijibu risala ya chama hicho kuhusu kupatiwa viwanja Arusha na Dodoma kwa ajili ya kujenga ofisi na ombi la kupatiwa Sh bilioni moja, aliagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha wanayafanyia kazi mapema.

# Johari asifu uboreshaji sheria ukuaji uchumi

Na Selemani Nzaro

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amesifu mageuzi ya kiuchumi yanayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia marekebisho ya sheria.

Johari alisema hayo Dodoma jana kwenye mkutano wa mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali na akahimiza mawakili wasimamie misingi ya kuanzishwa chama hicho ili wasimwangushe, Rais Samia.

Alisema marekebisho ya sheria zikiwemo Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sheria ya Uwekezaji, Sheria ya PPP, Sheria ya Kodi, Sheria ya Madini, Sheria ya Benki Kuu na sheria nyingine ambazo katika kipindi cha Rais Samia zimefanyiwa marekebisho na kuwa chachu ya ukuaji wa uchumi.

"Mimi naweza kuziweka sheria zote hizi na mabadiliko yote haya kwenye kapu moja zuri ambalo unaweza kuliita 'Mama Samia Doctrine of Law' ambayo ukipata mwandishi mzuri akaiandika na kuitafsiri kwa matendo yake ambayo ameyafanya katika kurekebisha sheria hizi ili zichagize ukuaji wa uchumi, ataandika makala nzuri ambayo itapendwa kusomwa na watu wengi," alisema Johari.

na kujadili maendeleo ya sekta ya sheria na kuidadavua Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Alifafanua kaulimbiu ya mkutano huo, 'Utawala wa sheria katika utekelezaji wa majukumu ya serikali ni nguzo muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050' akisema inawakumbusha mawakili wa serikali kusimamia vyema utawala wa sheria katika maeneo ya kazi.

"Aidha, inatukumbusha kama watumishi na viongozi wa umma kuzingatia sheria wakati wa kutekeleza majukumu bila kufanya uonevu. Inaweza kuwa vigumu kufikiria maendeleo ya Dira ya 2050 bila kuwepo mchango wa wanasheria," aliongeza Johari.

Alisema kupitia mkutano huo, chama kimeidhinisha mpango mkakati wa miaka mitano hali inayokifanya kuwa kikubwa baada ya kupitia mpango huo na kuuidhinisha na kuanza utekelezaji wa mpango huo.

Aidha, alisema mpango huo utatekelezwa vizuri kwa sababu haukutengenezwa ili uwekwe kwenye makabati na kwamba utatekelezwa kwa moyo na ari kubwa. Alisema viongozi watakaochaguliwa watauishi mpango huo.

Alisema ofisi ya Mwa-

mwandishi mzuri akaiandika na kuitafsiri kwa matendo yake ambayo ameyafanya katika kurekebisha sheria hizi ili zichagize ukuaji wa uchumi, ataandika makala nzuri ambayo itapendwa kusomwa na watu wengi," alisema Johari.

Alisema sekta ya sheria inaheshimu kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia ikiwa ni pamoja na ulezi wa chama hicho na ukuaji wa uchumi ambao ni mzuri na unaridhisha.

Johari alieleza kuwa malengo makuu ya mkutano huo ni kutoa fursa kwa wanachama kufahamu masuala yanayohusu chama pamoja

huo utatekelezwa vizuri kwa sababu haukutengenezwa ili uwekwe kwenye makabati na kwamba utatekelezwa kwa moyo na ari kubwa. Alisema viongozi watakaochaguliwa watauishi mpango huo.

Alisema ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kusimamia uundwaji wa kamati za kisheria za mikoa, wilaya na kliniki za kisheria zinazotoa huduma kwa wananchi bila malipo.

Alifafanua kuwa malengo ya kamati ni kupunguza mashauri yasiyo ya lazima dhidi ya serikali na kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi.



oagtanzania
www.oag.go.tz

HABARILEO JUMATANO APRILI 16, 2025

# Mawakili wa serikali watakiwa kuzingatia weledi utekelezaji Dira

Na Anastazia Anyimike

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amesema sekta ya sheria ina mchango mkubwa katika kusaidia serikali kufikia uchumi wa kati wa juu kupitia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 na kuwataka mawakili wa serikali kutimiza wajibu wao ipasavyo ili kufikia azma hiyo.

Akizungumza juzi wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa Chama cha Mawakili wa Serikali (PBA), Johari alisema mawakili wa serikali wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa weledi wakati wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 katika kutoa ushauri na utungaji wa sheria.

"Mawakili wa serikali wanapaswa kuwa wawezeshaji katika kuhakikisha serikali inaifikisha nchi kuwa na uchumi wa kati wa juu, lakini pia sisi tunaweza tukaharibu au kuivuta nchi nyuma tusipowajibika katika sheria tunazotunga, ushauri tunaoutoa na matendo yetu," alisema.

Aidha, Johari alisema mawakili wa serikali wana mchango muhimu katika kuhakikisha utawala wa sheria katika kutekeleza jukumu la serikali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2050.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kukifanya chama imara, chombo kikubwa ndani na nje ya nchi chenye mikakati ambayo itasaidia serikali kutekeleza malengo yake.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno alisema kupitia chama hicho, mawakili wa serikali popote pale walipo watakuwa huru kutekeleza majukumu kwa ujasiri, kwa ulinzi mkubwa na bila kutetereka.

Maneno pia aliwataka mawakili wa serikali kutokuwa na hofu au kuogopa kutoa ushauri pale wanapoona maslahi ya taifa hayalindwi.

"Niseme tutahakikisha tunafanya hivyo ili kuhakikisha kila mwanasheria kule aliko anatekeleza majukumu kwa niaba ya mwanasheria mkuu wa serikali kwani hakuna sababu ya kuwa na hofu, hakuna sababu kuogopa kutoa ushauri au kufika ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali.

"Hakuna hata sababu moja ya kuogopa, kuhofia kuifikia Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali au kutupigia simu hasa kama kuna jambo la dharura au maslahi ya taifa yatakuwa katika hatari ya kutolindwa," alisema.

Alisema kiu na maono ya mwanasheria mkuu wa serikali ni kuona mawakili wa serikali wanakuwa na mchango muhimu katika kuhakikisha dira ya taifa ambayo iko katika hatua mbalimbali itakapoanza inatekelezwa.

Kwa upande wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Shaban Abdallah aliwataka mawakili wa serikali kujua kuwa wao ni jeshi la kuiwezesha serikali kutekeleza majukumu yake kupitia sekta ya sheria.

Naye Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali nchini, Amedeus Shayo alisema mkutano ni fursa kwa mawakili wa serikali kujadili mambo yanayohusu maendeleo ya sekta ya sheria na changamoto zake.


TBC Digital
Kwa udl
TBC Digital UPDATES
Mawakili mkatende haki pasipo kujali maslahi binafsi
@tbc_online
tbcdigital@tbc.go.tz
#Usipitwe

OAG Tanzania
3d ·

*MAWAKILI WA SERIKALI WAPONGEZWA KWA KUTOA HUDUMA ZA KISHERIA BURE KWA WANANCHI*... See more

Like Comment Send Share



Home Jiachie Blog Mtaa Kwa Mtaa Blog MK Computer Tweaks

Michuzi Blog | MICHUZI TV

This Space can Only be yours
Call us today on +255 754 271 266

Habari Biashara Kimataifa Burudani Michezo Magazeti Zanzibar Michuzi TV Contact Us Zilizobamba

# MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AWATAKA MAWAKILI KUJADILI CHANGAMOTO ZA KISHERIA

MICHUZI BLOG AT MONDAY, APRIL 14, 2025 HABARI,

Na Janeth Raphael MichuziTv -Dodoma

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali,Hamza Johari,amewataka wanachama wa chama cha Mawakili,kutumia fursa ya mkutano Mkuu kujadili changamoto mbalimbali za kisheria ikiwemo kuzifanyia kazi.

Johari amesema hayo leo jijini Dodoma,wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa chama cha mawakili wa serikali,wenye lengo wa kujadili mustakabali wa chama hiko lakini pia kujitathmini utendaji kazi wao.

"Nawapongeza kwa kuandaa Mkutano huu naomba tumieni nafasi hii kujadili changamoto zilizopo ili kuzifanyia KAZI,"amesema Johari.

Mbali na hayo amemshkuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali,Samwe Maneno pamoja na menejimenti nzima ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,ikiwemo chama cha mawakili wa serikali,kutokana na kazi nzuri ya maandalizi ya Mkutano mkuu wa mwaka waliyofanya.



BONGO5

HABARI BURUDANI MICHEZO VIDEOS Log in Search for

# Hamza Johari akutana na uongozi wa Chama cha mawakili wa serikali

Yasini Ngitu · 3 days ago 2 minut

Facebook X



**OAG Tanzania**
2d ·

HABARI PICHA

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza S. Johari amekutana na Ujumbe kutoka Benki ya TCB plc uliomtembelea kwa lengo la kujitambulisha na kueleza huduma zinazotolewa na benki hiyo, tarehe 16 Aprili, 2025 Ofisini kwake Bungeni Jijini Dodoma.



OAG Tanzania
1d ·

*NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AFANYA MAZUNGUMZO NA UJUMBE WA BENKI YA TCB PLC*

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samweli M. Maneno amekutana na kufanya mazungumzo na Ujumbe kutoka Benki ya TCB Plc, Alhamis tarehe 17 Aprili, 2025 katika Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.



oagtanzania




View insights

Boost post

22

Liked by **leilamuhaji** and others

**oagtanzania** *MAWAKILI WA SERIKALI KUKUTANA DODOMA*.

oagtanzania




View insights

Boost post

oagtanzania




View insights

Boost post

61 2 1

Liked by **leilamuhaji** and others

**oagtanzania** *TPBA YAPATA RAIS MPYA*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora